



## **BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR**

### **MFUMO WA KUTUNUKU MATOKEO YA UPIMAJI/MITIHANI YA TAIFA KWA KUTUMIA WASTANI NA JUMLA YA ALAMA (DIVISHENI)**

#### **1.0 UTANGULIZI**

Baraza la Mitihani la Zanzibar limefanya maboresho ya mfumo wa kutunuku matokeo ya Upimaji/mitihani ya Taifa katika ngazi ya elimu ya Msingi na Sekondari ya awali. Mabadiliko hayo yamefanyika kufuatia maoni ya wadau wa elimu kuhusu haja ya kuwa na viwango bora vya ufaulu na madaraja yaliyo katika mfumo wa jumla ya alama (Divisheni) kwa elimu ya Sekondari ya awali pamoja na wastani kwa elimu ya msingi.

#### **2.0 UTARATIBU WA KUTUNUKU MATOKEO YA MITIHANI YA TAIFA**

Uchakataji wa matokeo ya Upimaji wa Kidato cha Pili utazingatia viwango vya alama, madaraja ya ufaulu na utaratibu wa matumizi ya alama endelevu (CA) kama inavyookenaka katika jadweli nambari:1:

##### **(a) Viwango vya ufaulu kwa Kidato cha Pili**

##### ***Jadweli nambari 1. Viwango vya Ufaulu kwa Kidato cha Pili***

<b>Daraja</b>	<b>Alama</b>	<b>Uzito wa daraja (Pointi)</b>	<b>Maelezo</b>
A	75-100	1	Nzuri Kabisa
B	65-74	2	Nzuri sana
C	45-64	3	Nzuri
D	30-44	4	Inaridhisha
F	0-29	5	Feli

**(b) Viwango vya Ufaulu kwa Elimu ya Msingi juu**

Uchakataji wa matokeo ya Upimaji wa elimu ya msingi utazingatia viwango vya alama, wastani wa ufaulu na utaratibu wa matumizi ya alama endelevu (CA) kama inavyookenaka katika jadweli nambari:2:

***Jadweli nambari 2. Viwango vya Ufaulu kwa Elimu ya Msingi Juu***

<b>Daraja</b>	<b>Alama</b>	<b>Maelezo</b>
A	81-100	Nzuri Kabisa
B	61-80	Nzuri sana
C	41-60	Nzuri
D	21-40	Inaridhisha
F	0-20	Feli

**(c) Viwango vya ufaulu kwa Elimu ya Msingi Awali**

Uchakataji wa matokeo ya Upimaji wa elimu ya Msingi Awali utazingatia viwango vya alama na madaraja ya ufaulu kama inavyookenaka katika jaduweli nambari:3

***Jadweli nambari 3. Viwango kwa Elimu ya Msingi Awali***

<b>Daraja</b>	<b>Alama</b>	<b>Maelezo</b>
A	81-100	Nzuri Kabisa
B	61-80	Nzuri sana
C	41-60	Nzuri
D	21-40	Inaridhisha
F	0-20	Feli

(d) **Madaraja ya Ufaulu**

- i. Madaraja ya Ufaulu yatakuwa katika mfumo wa Divisheni, Jumla ya Alama (Total Point Grading System) na wastani. Mtahiniwa aliyefanya masomo yasiyopungua 7 kwa Kidato cha Pili atatumikiwa Daraja la I, II, III au IV kwa kufuata jumla ya alama (Point) kama inavyookenaka katika jaduweli nambari:4:

***Jadweli nambari 4. Madaraja ya ufaulu kidato cha Pili***

<b>Daraja</b>	<b>Pointi</b>	<b>Maelezo</b>
I	7 -17	Nzuri Kabisa
II	18 -21	Nzuri sana
III	22 - 25	Nzuri
IV	26 – 28	Inaridhisha
0	29 -35	Feli

- ii. Mtahiniwa aliyefanya mtihani chini ya masomo saba kwa Kidato cha Pili atahesabiwa kuwa amefaulu kwa kiwango cha chini cha ufaulu wa daraja la Nne endapo atafaulu angalau masomo mawili katika Kiwango D au somo moja katika Kiwango A, B au C.
- iii. Aidha, mtahiniwa wa darasa la saba aliyefaulu kwa uzito wa wasatani wa “A” atahesabika kuwa ni **Kipawa**, uzito wa wastani wa “B” atahesabika kuwa ni **Mchepuo**, uzito wa wastani “C” atahesabika kuwa ni **Darasa maalum** na uzito wa wastani “D” na “F” atahesabika ufaulu wa **kawaida** kama inavyookenaka katika jaduweli nambari:5

*Jadweli nambari 5. Madaraja ya ufaulu kwa darasa la saba*

Daraja	Alama	Maelezo
A	81-100	Kipawa
B	61-80	Mchepuo
C	41-60	Darasa maalum
D	21-40	Darasa la kawaida
F	0-20	Darasa la kawaida

Kwa upande wa watahiniwa waliofanya mitihani ya Taifa ya Darasa la Nne ufaulu wao utakuwa katika mfumo wa **wastani (average)**.

Matumizi ya Alama Endelevu (CA) Uwiano baina ya alama endelevu (CA) na Alama za mtihani wa mwisho (FE) utakuwa ni **30:70**. Mchanganuo wa mchango wa alama 30 za CA kwa Kidato cha Pili na Darasa la Saba kama inavyookenaka katika jaduweli nambari:6:

***Jadweli nambari 6. Matumizi ya alama endelevu kwa kidato cha Pili  
na darasa la saba***

<b>FTEE na FOEE</b>		
<b>Aina ya upimaji</b>	<b>Alama</b>	<b>Maelezo</b>
Upimaji Kidato Cha Kwanza	10	Zinapatikana kutoka katika mtihani wa muhula wa I
Upimaji Kidato Cha Kwanza	10	Zinapatikana kutoka katika mtihani wa muhula wa II
Upimaji Kidato Cha Pili	10	Zinapatikana kutoka katika mtihani wa muhula wa I
Upimaji Kidato Cha Pili	70	Zinapatikana kutoka katika mtihani wa Taifa
<b>Jumla</b>	<b>100</b>	

**TANBIH:** 1. FTEE ni mtihani ya kuingia kidato cha tatu.

2. FOEE ni mtihani wakuingia kidato cha kwanza.

### **3.0 HITIMISHO**

Utaratibu wa kutunuku matokeo kwa muundo wa madaraja wa jumla ya alama (Divisheni) na wastani wa alama kwa Baraza la Mitihani la Zanzibar utaanza kutumika kwa mitihani ya Taifa ya mwaka 2022. Hivyo, ni matumaini ya Baraza kuwa mfumo huu utakuwa na tija na kufahamika vyema kwa wadau wa elimu na kupunguza changamoto na malalamiko ya matokeo.

**Imetolewa na:**

**Kitengo cha Habari na Uhusiano**

**Baraza la Mitihani la Zanzibar**